ST CHARLES COMMUNITY COLLEGE

TAASASI YA LUGHA YA KIINGEREZA

**Madarasa Ya Kiingereza Kama Lugha ya pili.**

Wanafunzi walio na visa ya kimasomo wanastahili wawe na alama sizizopungua 61 katika kipindi cha TOEFL IBT kwa minajili ya kujiunga na taaluma ya kiingereza kama lugha ya pili (ESL). Vilevile, wanastahili kuwa na alama 50 na kuzidi katika TOEFL IBT ili kujiunga na INE kiwango cha pili, pia uamuzi wa mwenyekiti (baada ya majaribio na idara ya ESL) ili kujiunga na INE kiwango cha kwanza. Wanafunzi ambao hawakufaulu kufikisha malengo yanayohitajika pia wanakubaliwa kujiunga kulingana na muhula, ila, wanastahili kuwa tayari kukaa zaidi ya muhula mmoja katika taasisi ya INE. Wanafunzi wote, bila kuzingatia alama zao za TOEFL ama IELT, huwa wanapaswa kufanya mtihani wa majaribio wa madarasa ya Kiingereza kama Lugha ya Pili (ESL) ambao unahusu kusoma, kuskiza, sarufi, insha, na mahojiano/ mazungumzo (kwa hali chache, insha, mahojiano/ mazungumzo na majaribio ya ofisini huenda yakawa ya kutosha). Wanafunzi wanahitajika kupata alama ya “C” ili kuhitimu kiwango kingine. Madarasa mengine huwa shuleni na mengine huwa mkondoni au kwenye mtandao.

*Kwa masharti yanayohitajika darasani, tembelea tovuti stchas.edu/ESL kwa maelezo Zaidi. Nambari iliyo kwa mabano inaashiria nambari ya michango ya kitaaluma ambayo kazi inapewa.*

**ESL 100: Mafanikio ya ujuzi wa wanafunzi katika SCC kwa wazungumzaji wa kiingereza wasio wa kiasili (NNS) (3)**
Masharti yaliyonoga kwa wanafunzi wanaozungumza kiingereza wasio wa kiasili kulingana na mikakati na ujuzi unaohitajika ili kuwa na mafanikio katika chou cha marekani, pamoja na kusikiliza, kuzungumza, kuandika maelezo, kuzingatia muda na mawasiliano yaliyoandikwa yanahitajika kwa wanafunzi walio katika mwaka wao wa kwanza katika chuo.

**ESL 103/SPE 100: Matamshi, kuzungumza, na kusikiliza kwa wazungumzaji wa kiingereza wasio wa kiasili (4)**
Masharti ya matashi kwa wazungumzaji wa kiingereza wasio wa kiasili. Kwa kuelimika lafudhi, uzani wa msongo wa silabi za kimarekani, wanafunzi wataeleweka zaidi.

**ESL 104/RDG 106: Masomo ya chuo kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (3)**
Maelekezo kwa ujuzi wa masomo ya chuo kwa kuzingatia msamiati, ufahamu, kufikiri kwa kindani, kusoma kwa ufanisi na kusoma kulingana na mtaala kwa wazungumzaji wasio wa kiasili.

**ESL 105: Mazungumzo ya kiwango cha juu kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (COM 101 Kifungu cha wazungumzaji wasio wa kiasili) (3)**
Lengo kwa uboreshaji wa mazungumzo na ujuzi wa kuwasilisha kwa njia yam domo kwa wazungumzaji wasio wa kiasili kwa kuzingatia ufasaha katika kuzungumza kiingereza, kuboresha ujuzi wa kusikiliza, na kanuni zinginezo za mawasiliano. Kumbuka: Sawa na COM 101 (Kwa wazungumuzaji wasio wa kiasili)

**ESL 106/RGD 106: Masomo ya kiwango cha juu  kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (3)**
Mazoezi ya kuelekezwa kwa ujuzi wa kusoma wa kiwango cha juu katika chuo kwa kusisitiza nidhamu maalum ya msamiati, ufahamu mwema, ujuzi wa kuchanganua wa kuwango cha juu, kusoma bora na kusoma kwa mtaala kwa wanafunzi ambao kiingereza ni lugha yao ya pili.

**ESL 107 (Iliyokuwa ESL 101): Mapitio ya sarufi kwa umakini kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (4)**
Mapitio ya sarufi na msamiati katika kiwango cha chuo kikuu kwa wanafunzi wa ESL, kwa kusisitiza dhana ya sarufi iliyolengwa, muundo wa sentensi na aya, msamiati, nahau na ujuzi wa kusoma.

**ESL 108 (Iliyokuwa ESL 102): Insha ya kiwango cha kati kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (NNS) (3)**
Maelekezo Zaidi kwa wazungumzaji wasio wa kiasili ili kuendeleza ujuzi wa kuandika wa kiwango cha chuo kikuu katika lugha ya kiingereza. Wanafunzi watazingatia ujuzi wa utunzi, aya, na ujuzi wa insha vilevile ujuzi wa sarufi.

**ESL 109: Uandishi wa utafiti na kufanya mtihani kwa wazungumzaji wasio wa kiasili (3)**
Wanafunzi watajenga ujuzi wa kutunga kwa kulenga ujuzi muhimu wa kuandika utafiti. Ujuzi wa kutumia maktaba, mitandao, kushirikisha utafiti kwa insha, sarufim na muundo wa sentensi.

**ESL 112: Msamiati wa kitaaluma kwa wanafunzi (1)**
Boresha msamiati wa kitaaluma Zaidi ya mafunzo ya kawaida katika somo la ESL 100. Chunguza maana matamshi, matumizi ya nambari za maneno kwa eneo la kozi ambalo laweza kushirikishwa kwa elimi ya kiujumla, ikiwa pamoja na sayansi, saikolojia, hisabati, fasihi, na mengineyo.

**ESL 113: Msamiati wa kiwango cha juu kwa madhumuni maalum kwa wazungumzaji wa kiingereza wasio wa kiasili**
Umakinifu katika kufunza wanafunzi msamiati kwa malengo ya kibinafsi au kwa eneo la kazi kwa hii kozi, watapenya kwa kina katika matumizi, maana, herufi, na mazingira ya maeneo maalumu misimu au sajili. Inapendekezwa kufanywa pamoja na ESL 299

**ESL 115: Jamii kama maabara ya darasani.**
Kozi hii inahusu maabara ya uandishi na mazungumzo ambayo hupeana juhudi Zaidi pamoja na dhana ngumu za darasani, kutokana kwa sarufi, msamiati, kuelekea kwa ufasaha na mazungumzo, vilevile safari za bararani, nafasi za kujijulisha na vyuo vingine, kufuzwa, wageni waheshimiwa, kufanya kazi kwa huru kwenye jamii na mazoezi kwenye jukwaa la kompyuta za masomo ya ESL. Ingawa warsha/maabara mengine huenda yakabadilika, kwa hii kozi, wanafunzi wanaweza jichagulia fursa zinazowavutia.

**ESL 116: Mazungumzo na matukio ya sasa katika kiingereza**

Maendeleo katika mazungumzo kulingana na matukio ya sasa, maswala ya kitamaduni na maendeleo ya kitaaluma, msamiati, sarufi inayozungumzwa, na ufahamu katika kusikiliza yatasisitizwa.

**ESL 120: Mafanikio katika kazi za huduma ya afya kwa wazngumzaji wasio wa kiasili. (3)**

Wazungumzaji wasio wa kiasili wanaojipanga kujiunga na mipango ya huduma za afya, katika vyuo vya marekani wanafaa wachukue somo hili. Somo hili husisitiza mazungumzo katika vifaa vya huduma za afya, kusoma vitabu vya huduma za afya, rekodi ya matibabu na utaaluma wa fasihi. Vilevile, kujifunza kwenye maabara na kliniki, kusomea istilahi za matibabu na kuwa na ujuzi katika utamaduni wa marekani katika sekta za afya.

**ESL 199: Utafiti wa tamaduni na jamii ya marekani (1)**

Kozi hii itaongeza ufahamu wa wanafunzi katika maswala ya kitamaduni, kijamii na kiuchumi, tofauti na njia za maisha kati ya marekani na nchi zingine. Kozi hii hutoa fursa za kutosha kwa wazungumzaji wasio wa kiasili kujifunza kuzungumza, kusikiliza, kusoma, na kuandika.

**ESL 290: Mazoezi kwa vitendo ya kitaaluma kwa lugha ya kiingereza.**

Uzoefu wa kindani kwa wanafunzi ili kuonyesha uwezo wa juu zaidi kwa lugha ya Kiingereza, vilevile kuutumia ujuzi wa lugha iliyopokelewa na yenye uzalishaji nje ya mazingira ya kitaaluma. Huu ujuzi wa kukitumia Kiingereza kwa kina waweza kuwa wa kujitolea au kujifahamisha na vyuo vingine kwenye jamii, au nje ya nchi ambapo Kizungu kinatumika. Ujuzi wa lugha zaidi zilizopatwa kando na mafunzo darasani zitahusisha nahau, mazungumzo, umahiri wa kitamaduni na msamiati zaidi pamoja na matarajio yaliyo thabiti na kiwango cha juu cha ESL 109/COM 101. Alama ya “C” ni kupita, ila “B” au bora inahitajika ili kuchangia kupata kwa cheti cha kizungu cha kitaaluma. Kozi inaweza fundishwa kwa chaguo la huduma za kusoma kwa baadhi ya maswala. Mwenyekiti huenda akaruhusu kazi kuwa na mbadala kwa moja ya kozi zinazohitajika kwa vyeti vya ESL vya kitaaluma.

**ESL 299: Taaluma ya Kizungu kwa madhumuni maalum**

Inalenga utumizi wa ujuzi wa ESL wa kusikiliza, kuandika, kusoma, na kuzungumza katika eneo maalum, kama vile biashara, saana ya upishi, na uhandisi. Mkazo kwa utumizi wa ujuzi wa lugha ya Kiingereza kwa mazingira yetu ya kila siku ambayo wanafunzi wa ESL watakumbana nayo kwa kazi zao. Inapendekezwa ufanywa pamoja na ESL 113.

**Mifano ya jinsi wanafunzi wa ESL huchukua kozi zao.**

Ufuatao ni mfano wa kiwango cha mwanafunzi wa ESL, lakini wanafunzi huenda wakawekwa kwa viwango tofauti kulingana na malengo yao, vilevile, ujuzi katika nyanja tofauti za kusoma, kuandika, kusikiliza, kuongea na maarifa ya kitamaduni.

| INE kiwango cha kwanza | INE kiwango cha pili | ESL kiwango cha kwanza | ESL kiwango cha pili (kilichokomaa) | ESL Kiwango cha tatu (Ujuzi) |
|---|---|---|---|---|
| ESL 100 (1) na ESL 199 (1) (kama | ESL 100 (3) na 199 (Ikiwa haikufanywa | ESL 100 na 199 (ikiwa haikufanywa | ESL 100 na 199 (ikiwa haukufanya | ESL 109 na 199 (ikiwa haikufanywa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| haikufanywa katika shule yetu) | katika shule yetu) | katika shule yetu) | katika shule yetu) | katika shule yetu) |
| INE 100 (9) | INE 102 (3) | ESL 103 (4) | ESL 105/COM 101 kwa wazungumzaji wasio wa kiasili | ESL 105 / COM 101 kwa wanafunzi ambao Kiingereza si lugha yao ya kiasili (ikiwa hukufanya hapo awali) |
| INE 112 (1) (yaweza kufanya muhula ujao) | INE 101 (3) | ESL 104 (4) | ESL 106 (3) | ESL 109 (3) |
| ESL 115 (0) | INE 111 (1) au INE 112 (1) ikiwa haikufanya katika shule yetu. | ESL 107 (4) | ESL 108 (3) | Teule za ESL |
| | ESL 115 (0) | ESL 115 (0) | ESL 115 (0) | ESL 115 (0) |
| | INE 199 (2) | Teule za ESL | Teule za ESL | Kozi za ujumla |
| | INE 190 (1-3) | Hisabati katika hali zingine. | Hisabati au kozi za ujumla/ ESL 120 kwa huduma za afya | ESL 120 kwa masomo ya huduma za afya ikiwa haikufanywa awali / hisabati/ kozi za ujumla. |
| | | | ESL 299 Kizungu kwa sababu maalum (bishara, uhandisi na zinginezo) | ESL 299 Kizungu kwa sababu maalum kama vile bishara na zinginezo. |

KARIBISHO

1. Kwa maswala kuhusu kozi za fasihi ya kiingereza, wasiliana na Dr. Dawn Huffman, mwenyekiti wa kozi za fasihi ya kiingereza chuoni katika nambari 636-922-8574 au dhuffman@stchas.edu (bora ukitumia wasifu badala ya nambari)
2. Wanafunzi wajazi wanastahili kujiandikisha kwenye chuo cha mafunzo kwa tovuti stchas.edu ili wapate nambari yao ya uanafunzi, na kushiriki sehemu ya kwanza ya tathmini za ESL (walete kitambulisho). Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti: stchas.edu/assessment.
3. Hata hivyo, wanafunzi wa kimataifa wanaotaka kufanya uteuzi kulingana na mahitaji na taratibu za kuhudhuria SCC wanastahili kutembelea tovuti stchas.edu/internationalappointment na kuchagua chaguo la 'international student support'. Wanaweza wasiliana na Laurie Bernady, ambaye ni mtaalumu wa usaidizi wa wanafunzi wa kimataifa kwa nambari 636-922-8611 au kuandika wasifu kwa lbernardy@stchas.edu. Kwa sasa, eneo la usaidizi wa wanafunzi wa kimataifa liko katika "College Center" chumba cha 102. Wanafunzi wa kimataifa wanaotaka kujiunga nasi wanaeza tembelea tovuti ya stchas.edu/internationalstudies kwa maelezo zaidi.
4. Kwa kufanya uteuzi wa ESL baada ya kufanya tathmini ya ESL wanafunzi wote wanastahili kutembelea tovuti ya stchas.edu/internationalappointment na kuchagua "ESL Interview/Advising".
5. Wanafunzi wote wanastahili kuuliza kuhusu uwezekano wa kupata cheti cha misingi ya Kiingereza au cheti cha utaalamu katika ESL.

PICTURE

Taaluma ya lugha ya Kiingereza inawezesha wanafunzi kujifunza Kiingereza kwa sababu mbalimbali, kutoka kwa kazi na matayarisho katika elimu kuelekea kwa kujifunza kwa muda mrefu na uwakili wa kijamii. Taaluma ya ESL na vipindi vya lugha vinapendekeza utofauti, vilevile mafanikio ya mwanafunzi.

St Charles Community College na mazingira yao ya kupendeza na usalama katika mji wa Cottlevile, Missouri nchi ya marekani inakaribisha wanafunzi wa kimataifa, wakazi na wageni wanaotembelea shule yetu ambao Kiingereza si lugha yao ya kiasili. Tunawapa wanafunzi wetu rasilimali za kuwasaidia katika chuo na kuendelea katika kazi ambazo watafaidi kutoka mazungumzo, maandishi, masomo, na kusikiza katika lugha ya Kiingereza. Ustadi huu wote hufunzwa katika madarasa yetu yote.

Walimu na maprofesa wetu wana ujuzi wa kufunza wanafunzi wasio wa kiasili, na mafunzo yetu yameundwa ili masomo kufanyika ndani na nje ya darasa. Tuna vipindi viwili, Kiingereza kwa undani (INE) kwa kiwango cha chini hadi masomo ya juu kidogo, na taaluma ya Kizungu kama lugha ya pili (ESL) kwa kiwango cha juu kidogo hasi kiwango cha juu zaidi. SCC inapeana masomo ya taaluma za mikopo, cheti cha misingi ya Kiingereza (kwa wanafunzi wa INE) na vyeti vya utaalamu wa kiwango cha juu cha ESL, ambavyo vinarudishwa kwa taasisi ya masomo kama ushahidi wa kufanikiwa katika Kiingereza. Kwa hivyo, ingawa wanafunzi wamekuja kwenye nchi au wameishi kwa muda mrefu, SCC inataka kuwasaidia katika masomo yao.